

TOLEO LA 27

Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule za Kaunti ya DeKalb,

Ninawakaribisha kwa furaha wasomi wetu ambao wamechagua masomo ya ana kwa ana wanaporudi kwenye majengo! Mwaka huu uliopita umekuwa na changamoto wakati tulipokabiliana na janga la ulimwengu la COVID-19. Tumepata hasara kama jamii na taifa. Hata hivyo, tunapokaribia kurejea hali ya kawaida, nina matumaini kwamba tutakuwa wenye nguvu na ubora zaidi kuliko hapo awali.

Ingawa ninafurahia kuhusu tarehe 9 Machi, ninatazamia siku ambayo tutakaribisha salama wasomi wetu WOTE kurudi kwenye majengo yetu. Hadi siku hiyo, tutajitahidi kwa bidii ili kuhakikisha wasomi wetu wanafanikiwa katika awamu ya masomo mahuluti.

Mikakati ya Kupunguza Hatari

Usalama na ustawi wa wanafunzi, walimu na wafanyakazi wetu ni wa umuhimu mkubwa na unabaki kuwa kipaumbele cha juu. Wakati wanafunzi wetu, walimu na wafanyakazi wanaanza kutumia majengo, mikakati ya kupunguza hatari— inayopendekezwa na Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) - itatekelezwa ili kuhakikisha kuwa kila mtu yuko salama. Mikakati ambayo Wilaya inatekeleza ili kupunguza hatari ya maambukizi ni pamoja na:

- Kuvaa barakoa wakati wote
- Kuweka umbali wa kimwili
- Kunawa mikono yako
- Kusafisha na kutakasa
- Ufuatiliaji wa watu waliotangamana kwa karibu na aliyeambukizwa
- Kujenga mfumo wa upitishaji hewa safi

Kwa maelezo zaidi kuhusu jinsi tunavyoweka salama Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb, bofya [hapa](#). Ili uone njia za basi, bofya [hapa](#).

Chanjo ya COVID-19

DCSD inashirikiana kwa karibu na Bodi ya Afya ya DeKalb katika mkakati wa utekelezaji kwa wafanyakazi ili wapokee chanjo ya COVID-19 mara tu usambazaji mkubwa wa chanjo unapopatikana. Maelezo zaidi yatatolewa wiki ijayo. Wafanyakazi pia wanahimizwa kuwasiliana na mtoa huduma wao msingi ili kujua upatikanaji wa chanjo.

Hongera

Wiki iliyopita DCSD ilipata habari nzuri sana! Ningependa kumpongeza mwanafunzi wa mwaka wa mwisho wa Shule ya Upili ya Lithonia [Zae Brewer](#), ambaye alichaguliwa kama mjumbe wa Georgia katika Mpango wa Vijana wa Seneti ya Marekani ya 2021 (USSYP). Atajiunga na wajumbe wanafunzi 104 na atapata udhamini wa \$10,000 wa chuo kikuu kwa masomo ya shahada ya kwanza. Tunajivunia Zae, na tunajua atawakilisha Lithonia High na DCSD vizuri!

Ningependa pia kupongeza shule 11 za upili ambazo zilitajwa katika [Advanced Placement \(AP\) Honor Schools!](#) Madarasa ya AP huwapa wasomi wetu fursa ya kujifunza maudhui katika kiwango cha chuo kikuu wakati wamo shule ya upili na kufanya mitihani ya AP inayotolewa na Bodi ya Chuo. Hongera sana waalimu, wafanyakazi na wasomi katika Shule ya Upili ya Arabia Mountain, Shule ya Upili ya Chamblee Charter, Shule ya Upili ya Clarkston, Shule ya Upili ya Cross Keys, Shule ya DeKalb Early College, Shule ya Sanaa ya DeKalb, Shule ya Upili ya Druid Hills, Shule ya Upili ya Dunwoody, Shule ya Upili ya Lakeside, Shule ya Upili ya Southwest DeKalb na Shule ya Upili ya Tucker kwa heshima hii kubwa!

Wiki ya Kutoa Shukrani kwa Bodi

DCSD inajiunga na wilaya zingine za shule kote katika jimbo wakati wa mwezi wa Machi kusherehekea Wiki ya Kutoa Shukrani kwa Bodi ya Shule ya Georgia mnamo Machi 15-19. Tunawaheshimu washirika wa bodi ya shule yetu kwa kujitolea kwao kuwahudumia wanafunzi, wafanyakazi, wazazi na wadau wengine wa Wilaya.

Tunawashukuru washirika Bodi ya Elimu kwa kuwa na ujasiri wa kushiriki katika majadiliano magumu na kufanya maamuzi magumu kwa ajili ya maendeleo ya wanafunzi wetu. Tunawashukuru pia kwa utawala wao na jukumu lao katika kupigania

na kutetea elimu bora kwa wanafunzi wote.

March Mindfulness

DCSD ilifanikiwa kuanza "March Mindfulness" kwa wafanyakazi wiki iliyopita. Mpango huu muhimu unaruhusu wafanyakazi kushiriki katika vikao vya dakika 30 ambavyo vinalenga kutumia zana zinazotegemea ushahidi ili kudhibiti mafadhaiko, kutuliza akili na kushughulikia uchovu. Tulipokea maoni mazuri kutoka kwa wafanyakazi wetu wachache kuhusu kikao cha kwanza, na tunawahimiza wafanyakazi wote kushiriki katika kikao, ambacho kinatolewa na Bw. Curtis Smith, Mwanzilishi wa Moment of Mindfulness.

Ninatazamia kusikia kusikia kuhusu hadithi zaidi za kufaulu za wanafunzi, walimu na wafanyakazi wetu!

Wako mwaminifu,

Bi. Cheryl Watson-Harris